

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA**

**19 MEI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA– TAREHE 19 MEI, 2021

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **263. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka vivutio maalum ili kuvutia Wawekezaji kwenye Viwanda vya kubangua Korosho.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **264. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na changamoto ya huduma za afya katika Zahanati zetu hasa ukosefu wa dawa pamoja na huduma bure kwa Wazee, Watoto na Akina mama wajawazito:

Je, ni lini Serikali itahakikisha Sera ya Afya inatekelezwa bila tatizo lolote.

**265. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaweka Vifaa vya Maabara kwenye Maabara zote za Shule za Sekondari katika Wilaya ya Mkalama zilizojongwa kwa nguvu za Wananchi.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**



**266. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, nini Mpango wa Serikali kuhakikisha kuwa Timu ya Taifa Stars inafanya vizuri katika Michezo ya Kimataifa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **267. MHESHIMIWA STANLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Maswa hadi Lalago.

### **268. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mhe. Rais ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Shigamba kwa kiwango cha lami.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **269. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitangaza Hifadhi ya Taifa ya Katavi.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **270. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itatoa uamuzi wa kuwaruhusu Wavuvi wa Kamba Koche kuvua kuanzia Mwezi Desemba hadi Julai kila Mwaka.

## **WIZARA YA NISHATI:**

### **271. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Wilaya ya Tanesco kwa ajili ya kuhudumia Viwanda na Wananchi katika Mji wa Mafinga ili kuendana na kasi ya Uchumi wa Viwanda.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA  
YA HABARI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA  
19 MEI, 2021**

**S.KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**